# HALMASHAURI YA MJI WA BABATI

## MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI YA MJI TAREHE 20.10.2021

MAHUDHURIO YA WAJUMBE

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Bi.Rena S. Urio | Mwenyekiti |
| 2. | Bi. Amida M. Lema | Katibu |
| 3. | Bi Pascalina Lowokelo | Mjumbe |
| 4. | Bw. Sadik S. Mrisho | Mjumbe |
| 5. | Bw. Khamisi J. Katimba | Mjumbe |
| 6. | Bi. Irene M. Kasonga | Mwanasheria |

SECRETARIAT

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Bw. Mohamed Khatib | Secretariat |
| 2. | Bw. Gift Rwetoijela | Secretariet |

WAALIKWA

| | | |
|---|---|---|
| i. | Bw. J. Shimi Emanuel | Mweka hazina (T.T.) |
| ii. | Bw. Nicholous Nnlula | Afisa Bajeti. |
| iii. | Eng. Franco Kapinga | Kaimu Mkuu wa Idara ya ujenzi. |

**BTC/CTB/MUHT.NA.07/10/2020-2021: KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti alifungua Kikao Mnamo saa mbili na nusu (02:30) asubuhi na aliwakaribisha wajumbe na waalikwa kwenye kikao. Aidha aliwaeleza wajumbe kuwa Katibu wa Bodi ya zabuni Bi Amida M.Lema anatarajia kustaafu utumishi wa Umma hivi karibuni hivyo anaaamini hiki ni kikao chake cha mwisho kwenye Bodi ya zabuni.

**BTC/CTB/MUHT.NA.08/10/2020-2021: KUSOMA NA KUTHIBITISHA AGENDA ZA KIKAO CHA TAREHE 20.10.2021**

Katibu aliwasilisha agenda za kikao. Wajumbe walizipokea na kuthibitisha kuwa ni agenda za kikao cha siku hiyo.

Agenda zilikuwa kama ifuatavyo:

1) Kufungua kikao.
2) Kuthibitisha agenda za kikao cha tarehe 20/10/2021.
3) Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha tarehe 03/08/2021.
4) Yatokanayo na Muhtasari wa kikao cha tarehe 03/08/2021.
5) Pendekezo la Kuhuisha Mpango wa Manunuzi wa Halmashauri wa Mwaka wa Fedha 2021/2022 kwa kuingiza fedha zilizopokelewa nje ya Bajeti.
6) Pendekezo la kuridhia Manunuzi yaliyofanyika kwa kutumia Masurufu (Imprest).
7) Taarifa ya Manunuzi yaliyofanyika kwa *circular Resolution* kwa kipindi cha Mwezi Julai hadi Septemba 2021.
8) Pendekezo la kuridhia njia ya manunuzi kwa ajili ya kutekeleza wa miradi ya maendeleo kwa bajeti ya 2021/2022 na fedha zilizopokelewa nje ya bajeti.



CamScanner

9) Mengineyo kwa idhini ya mwenyekiti.
10) Kufunga kikao.

**BTC/CTB/MUHT.NA.09/10/2020-2021: KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 03/08/2021.**

Muhtasari wa kikao cha tarehe 03.08.2021 ulisomwa na wajumbe waliridhia na kuthibitisha kuwa ni kumbukumbu sahihi ya ofisi.

**BTC/CTB/MUHT.NA.10/10/2020-2021: YATOKANAYO NA MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI CHA TAREHE 03.08.2021**

Yatokanayo na muhtsari wa kikao cha tarehe 03.08.2021 yaliwasilishwa. Katibu aliwaeleza wajumbe kwa kurejea kikao cha tarehe 03.08.2021 ya kwamba Bodi ya zabuni iliridhia kuanza kwa ujenzi wa kituo cha Afya Singu kwa njia ya Manunuzi ya kikosi kazi (Force Account) kwa Majengo yote saba (07) ambapo ujenzi utaanza kwa Majengo mawili ambayo ni jengo la wagonjwa wan je (OPD) na Wodi ya wazazi (Maternity Ward) kwa gharama ya Tshs.361,411,698.00.Hata hivyo bakaa ya Tshs. 38,588,302 zilielekezwa kujenga Miundombinu mingine itakayowezesha kituo kufunguliwa.

**Utekelezaji wake:** Kwa sasa ujenzi wa kituo cha afya singu umeanza na ujenzi wa Majengo mawili ambayo ni jengo la wagonjwa wanje (OPD) na Wodi ya wazazi (Maternity Ward) kwa sasa kazi inaendelea. Wajumbe walipokea na kujadili na walielekeza kazi iendelee.

**BTC/CTB/MUHT.NA.11/10/2020-2021:PENDEKEZO LA KUHUISHA MPANGO WA MANUNUZI WA HALMASHAURI WA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 KWA KUINGIZA FEDHA ZILIZOPOKELEWA NJE YA BAJETI.**

Katibu aliwasilisha pendekezo la kuhuisha Mpango wa Manunuzi wa Halmashauri kwa mwaka wa Fedha 2021/2022 kwa Kwa kuingiza Fedha zilizopokelewa nje ya Bajeti jumla ya Tshs.1,056,615,745.33 zikiwa kwa ajili ya shughuli za Miradi ya Maendeleo kwa mchanganuo ufuatao:

| SEKTA | MRADI | KIASI |
|---|---|---|
| Elimu Msingi | Ujenzi wa Matundu ya vyoo na Mifumo ya maji | 68,544,759.7 |
| Elimu Sekondari | Ujenzi wa jengo la Utawala na Mifumo ya maji | 61,872,379.85 |
| Afya | Ujenzi wa kituo cha Afya | 250,000,000. |
| **Jumla ndogo** | | **396,615,745.33** |

Halmashauri inatarajia kupokea Fedha za mpango wa Ustawi wa Jamii na Mapambano dhidi ya COVID -19 kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ifuatayo:

| SEKTA | MRADI | KIASI |
|---|---|---|
| Elimu Msingi | Ujenzi wa Madarasa mawili (02) shule shikizi | 40,000,000. |
| Elimu Sekondari | Ujenzi wa madarasa kumi na sita (16) | 320,000,000. |
| Afya | Ujenzi wa Jengo la Wagonjwa wa dharura | 300,000,000 |
| **JUMLA KUU** | | **1,056,615,745.33** |



CS CamScanner

Wajumbe walipokea na kujadili. Aidha Afisa Bajeti pamoja na mweka Hazina walitoa maelezo mafupi pamoja na kuwahakikisha wajumbe kuwa takwimu za kiasi cha fedha kilichopokewa ni sahihi. Baada ya majadiliano na ufafanuzi kutolewa, Bodi ya zabuni iliamua yafuatayo:

1. Bodi ya zabuni iliridhia Mpango wa Manunuzi wa Halmashauri uhuishwe kwa kuingiza kiasi cha fedha Tshs.1,056,615,745.33 zilizopokelewa nje ya Bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022.
2. Taarifa hii iwasilishwe kwenye kikao cha Kamati ya Fedha na uongozi kwa ajili ya kupata ridhaa.

**BTC/CTB/MUHT.NA.12/10/2020-2021: PENDEKEZO LA KURIDHIA MANUNUZI YALIYOFANYIKA KWA KUTUMIA MASURUFU (IMPREST).**

Mwenyekiti alimkaribisha mweka Hazina ili aweze kuwasilisha agenda hii. Mweka Hazina aliwaeleza wajumbe kuwa anawasilisha agenda hii ili Bodi ya zabuni iweze kuridhia manunuzi ambayo yalifanyika kwa kutumia Masurufu kwa sababu mbali mbali zikiwamo uharaka. Aidha manunuzi hayo yanahusisha ununuzi wa FAX Machine wakati wa uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 na matengenezo/ukarabati wa stendi Kuu ya Mabasi. Hivyo anawasilisha manunuzi haya ili Bodi ya zabuni iweze kuridhia na kuwa kumbukumbu za ofisi.

Mchanganuo wa manunuzi hayo ni kama ifuatavyo:

1) Ukarabati/ Matengenezo ya kituo Kikuu cha Mabasi (Maisaka Katani) Tshs. 27,520,000 kwa mwaka wa fedha 2021/2022.
2) Ukarabati/Matengenezo ya kituo Kikuu cha Mabasi (Maisaka Katani) Tshs. 26,780,000 2020/2021.
3) Ununuzi wa FAX Machine wakati wa uchaguzi Mkuu Tshs.700,000/=

Wajumbe walipokea na kujadili.Aidha wajumbe walitaka kufahamu sababu zilizopelekea manunuzi hayo kutofuata taratibu za Manunuzi.

Kaimu Mkuu wa Idara ya ujenzi alieleza kuwa sababu ni pamoja na uharaka ikizingatiwa stendi ni chanzo kikubwa cha mapato katika Halmashauri yetu. Hata hivyo alieleza wakati mwingi inalazimika kuchukua Masurufu kutokana na hali halisi ikiwamo wenye vyombo vya usafiri kutishia kugoma kuingia stendi pamoja na uwepo wa mvua.

Kuhusu ununuzi wa FAX machine, Mweka hazina aliwaeleza wajumbe kuwa hii ilikuwa ni hitaji la haraka na endapo tungechelewa kuipata ingepelekea kukwamisha zoezi la uchaguzi. Baada ya majadiliano na ufafanuzi kutolewa Bodi ya zabuni iliamua yafuatayo:



CamScanner

i. Kwa kuzingatia umuhimu wa kazi tajwa na kifaa kilichonunuliwa,Bodi ya zabuni iliridhia Manunuzi hayo.
ii. Bodi ilielekeza wakati mwingine taratibu za Manunuzi zizingatiwe.
iii. Bodi ilielekeza kazi ya Matengenezo/ ukarabati unaendelea stendi uzingatie ubora kwa lengo la kupata thamani ya Fedha.
iv. Bodi ya zabuni ilielekeza kifaa (FAX Machine) iingizwe kwenye vitabu vya Leja na kuwekewa namba za utambulisho (Codefication).

BTC/CTB/MUHT.NA.13/10/2020-2021:Taarifa ya Manunuzi yaliyofanyika kwa *circular Resolution* kwa kipindi cha Mwezi Julai hadi Septemba 2021.
Katibu aliwasilisha taarifa ya ambayo Bodi ya zabuni iliidhinisha kwa *circular Resolution* ili Bodi ya zabuni iweze kuridhia na kuwa kumbukumbu za ofisi. Manunuzi hayo ni kama ifuatayo:

a) Manunuzi Mtambuka kama shajala, mafuta ya magari, chakula na viburudisho Tshs.199, 787,144.
b) Mkataba wa kutoa huduma ya ulinzi kwa mwaka wa fedha 2021/2022 (Octoba – Juni 2022), M/S Mputa Security Guard Sevices Co. Tshs.36,000,000
c) Mkataba wa kutoa huduma ya usafi kwa mwaka wa wa fedha 2021/2022 (Octoba –Juni 2022) Tshs. 42,250,000.
Wajumbe walipokea na waliridhia kuwa ni maamuzi sahihi ya Bodi ya zabuni hivyo ni kumbukumbu ya ofisi.

BTC/CTB/MUHT.NA.14/10/2021-2022: PENDEKEZO LA KURIDHIA NJIA YA MANUNUZI KWA AJILI YA KUTEKELEZA WA MIRADI YA MAENDELEO KWA BAJETI YA 2021/2022 NA ZILIZOPOKELEWA NJE YA BAJETI
Katibu alianza kuwasilisha kwa kuwaeleza wajumbe kuwa Halmashauri imekuwa ikipokea fedha zikiwamo fedha za bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na zilizopokelewa nje ya Bajeti jumla ya Tshs.1,056,615,745.33 zikiwa kwa ajili ya shughuli za Miradi ya Maendeleo. Hivyo aliomba mweyekiti aweze kuruhusu mwakili shi wa Idara ya Mpingo aweze kueleza zaidi.
Mwakilishi wa Idara ya Mipango (Afisa Bajeti) aliwaeleza wajumbe kuwa Halmashauri imepokea jumla ya Tshs.1,056,615,745.33 zikiwamo fedha za COVID -19 zikiwa ni kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi mbalimbali ya Maendeleo kama mchanganuo ulivyo katika Muhtasari Na. 11 hapo juu. Aliendelea kuwaeleza wajumbe kuwa katika kikao kilichofanyika Mkoani, Mkuu wa Mkoa na Katibu Tawala walielekeza na kusisitiza kuwa Miradi yote iwe imekamilika ifikapo tarehe 15 mwezi Desemba 2021

Kuhusu Manunuzi ya vifaa Mkoa ulielekeza vifaa kama Sementi, Bati, Nondo, Tiles, Mbao Rangi vinunuliwe moja kwa moja viwandani. Aidha vifaa vingine mchanganyiko vinunuliwe kwa wazabuni walioidhinishwa na GPSA kwa kufanya ushindanishi (Min Competition Quotation). Hata hivyo alisitiza sana kuzingatia bei ya soko. Vile vile



CS CamScanner

kamati za ujenzi na wote watakaohusika katika utekelezaji wa Miradi hii wawe waadilifu na waaminifu kwa lengo la kuhakikisha thamani ya Fedha inapatikana (VFM).
Wajumbe walipokea na kujadili na waliamua yafuatayo:

i. Maelekezo ya yaliyotolewa na Mkoa yazingatiwe.
ii. Vifaa kama Sementi, Bati, Nondo, Tiles, Mbao Rangi vinunuliwe moja kwa moja viwandani.
iii. Bodi ya zabuni ilimwagiza Kaimu Mkuu wa Idara ya ujenzi aandae BOQ mbili, Moja kwa kila Mradi, ya pili ni Mahitaji ya vifaa tajwa kwa Miradi yote na iwasilishwe kwa RAS kwa ajili ya vifaa hivyo kununuliwa viwandani.
iv. vifaa vingine mchanganyiko vinunuliwe kwa wazabuni walioidhinishwa na GPSA kwa kufanya ushindanishi (Min Competition Quotation).
v. Idara kama Mipango, PMU, Elimu Msingi na Sekondari wahakikishe wanazishauri wanafuatilia, kusimamia utekelezaji wa miradi hii ikiwa ni pamoja na kutoa ushauri kwa Kamati za ujenzi.
vi. Bodi ya zabuni iliridhia njia ya Manunuzi ya kikosi kazi (Force Account) kutumika katika ujenzi wa Miradi hii.

**BTC/CTB/MUHT.NA.12/10/2020-2021: MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI**

Mwenyekiti aliwaeleza wajumbe kuwa, Katibu wa Bodi Bi. Amida M. Lema anastaafu hivi karibuni. Hivyo kwa niaba ya Bodi ya zabuni alimshukuru kwa kazi nzuri. Aidha alitoa Mfano wakati wa utekelezajiwa Mradi wa ULGSP ya kwamba akiwa kama Mkuu wa Kitengo cha manunuzi aliweza kusimamia sheria ya ununuzi wa umma na kupelekea Halmashauri yetu kupata barua pongezi iliyotolewa na PPRA. Hivyo aliwasisitiza PMU kuhakikisha wanaendelea kufanya kazi kwa weledi. Aidha Bi Amida M. Lema aliishukuru Bodi ya zabuni, PMU na Watumishi wote wa Halmashauri ya Mji wa Babati kwa ushirikiano na waliompa kwani alieleza peke yake asingiweza.

**BTC/CTB/MUHT.NA.13/10/2020-2021: KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa michango mizuri ya mawazo. Mwenyekiti alifunga kikao mnamo saa nne na dakika arobaini na tano (04:45) asubuhi.

**UMETHIBITISHWA**

| | |
|---|---|
| ........................... | ........................... |
| Bi. Rena S. Urio | Bi.Amida M. Lema |
| MWENYEKITI | KATIBU |

20/10/2021
TAREHE



CamScanner